SCHOOL BASED ASSESSMENT

KISWAHILI
SEHEMU B

(For Regular Learners and Learners with Physical Disability)

Gredi ya 4 – 2026

JINA LA MWANAFUNZI : _____ **GREDI :** _____

NAMBARI YA TATHMINI:_____

TAREHE:_____

JINA LA SHULE: _____

KWA MATUMIZI YA MTAHINI

JEDWALI LA ALAMA

	ZOEZI 3: **UFAHAMU WA KUSOMA**	**ZOEZI 4:** **SARUFI**	**ZOEZI 5:** **KUANDIKA**
Swali	**1-16**	**17-30**	**31**
Upeo	**16**	**14**	**10**
Alama za mwanafunzi			
Kiwango Cha Utendaji			

Tathmini hii ina kurasa 9 zilizopigwa chapa.

Geuza ukurasa

ZOEZI 3: UFAHAMU WA KUSOMA

Swali la 1 hadi la 4

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Baada ya kufunga shule, Rehema alimtembelea nyanya yake. Alimpelekea matunda na mboga. Nyanya alimkaribisha kwa furaha. Rehema alimwambia kwamba angekaa kwake kwa muda wa wiki moja. Nyanya alifurahi sana.

Rehema alimsaidia Nyanya kufanya kazi. Kila siku, waliamka asubuhi na mapema kutayarisha kiamsha kinywa pamoja. Baada ya kiamsha kinywa, Rehema na Nyanya walielekea shambani. Nyanya alipokuwa akipalilia, Rehema alifurahia kung'oa magugu. Nyanya alifurahishwa na bidii ya Rehema. Kutokana na bidii ya Rehema, Nyanya alimfunza kupika vyakula vya kiasili kama vile mihogo, viazi vitamu na kunde.

Mara kwa mara, Nyanya alimtambia Rehema hadithi na kumpa **mawaidha**. Alimshauri kuwaheshimu wakubwa wake, kuwa mtiifu na kuwasaidia wazazi wake kufanya kazi za nyumbani. Pia, alimkumbusha kuzingatia bidii masomoni na kujiepusha na marafiki wabaya. Rehema alijifunza mengi wakati wa likizo hiyo.

1. Rehema alimpelekea Nyanya nini alipomtembelea?

   _____

2. Rehema alionyesha bidii kwa njia gani?

   _____

3. Je, unafikiri Nyanya alifanya nini Rehema alipokuwa akiondoka?

   _____

4. Neno **mawaidha** limetumika katika kifungu. Andika neno lingine lenye maana sawa na **mawaidha**.

   _____

Swali la 5 hadi la 8

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Hapo zamani za kale, baadhi ya wanyama walikuwa na mikia mirefu. Hata hivyo, mkia wa Sungura ulikuwa maridadi kuliko ya wanyama wengine. Jambo hili lilimfanya kujaa maringo. Wanyama walimuonya awache maringo bali hakuwasikiliza.

“ Nyinyi mnanionea wivu tu,” Sungura aliwajibu kwa kiburi.

Siku moja, mfalme Simba alitanganza mashindano ya mbio. Wanyama wote walialikwa. Sungura alijiambia angewashinda wanyama wote kwani yeye ni mwepesi. Wanyama waliingoja siku hiyo kwa hamu.

Siku ya mashindano ilipofika, wanyama wote walikusanyika pamoja. Mashindano yalianza asubuhi. Sungura alikimbia kwa kasi mno. Aliruka kwa maringo. Aliingia kichakani akidhani atapata njia rahisi. Kwa bahati mbaya mkia wake ulishikwa kwenye mwiba. Alijaribu kujitoa haraka ili wanyama wengine wasimpite lakini hakufaulu. Sungura aliendelea kuuvuta mkia wake kwa nguvu. Salaale! Mkia wake ulikatika ukabaki kipande kifupi tu.

“ Mkia wangu! Mkia wangu!” Sungura alilia. Aliendelea kukimbia lakini wanyama wengine walikuwa **wamemtangulia** kufika. Wanyama walishangaa kumwona Sungura akiwa wa mwisho. Walishangaa zaidi kumwona akiwa na mkia mfupi. Sungura alitembea kwa aibu na huzuni. Wanyama walimhurumia.

5. Kulingana na aya ya kwanza, jambo gani lilimfanya Sungura kuwa na maringo?

   _____

6. Katika kifungu, ni jambo gani linaloonyesha kuwa Sungura ni mwenye kujiamini?

   _____

7. Je, unadhani wanyama wengine walijifunza nini kutokana na tabia ya Sungura?

   _____

8. Neno,**wamemtangulia** limetumika katika kifungu kumaanisha

   _____

Swali la 9 hadi la 12

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Siku ya kusherehekea kuzaliwa kwa Bahati ilipofika, wazazi wake walimpeleka kwenye Mbuga ya Wanyama ya Bondeni. Asubuhi hiyo, Bahati alijitayarisha akiwa mwenye furaha tele. Alikuwa ametamani kuwaona wanyamapori kwa muda mrefu. Hii ni kwa sababu alikuwa akiwaona tu kwenye picha.

Walipofika kwenye lango la kuingia mbugani, walijiandikisha. Punde tu, Bahati aliwaona nyani wakirukaruka kwenye miti. Aliwakodolea macho kwa mshangao. Mwelekezi wao alianza kuwatembeza. Bahati alitaka kuwapa nyani hao ndizi. Aliponyoosha mkono tu, mwelekezi alimkataza. Alimweleza kuwa hawaruhusiwi kuwapa wanyama wa mbugani vyakula. Bahati alimsikiliza kwa makini.

Waliingia kwenye gari la kuwatembeza mbugani. Gari hilo lilikuwa na nafasi pana ya kutazama nje. Bahati alisimama na kujionea ndovu wengi. Aliwaona pia twiga na nyumbu. Baadhi walikuwa wakila majani huku wengine wakitembea. Mnyama aliyemfurahisha Bahati zaidi ni fisi. Bahati alikuwa amesoma hadithi nyingi kuhusu fisi. Wakati huo wote wazazi wa Bahati walikuwa wametulia garini wakitazama nje. Haikuwa mara yao ya kwanza kuzuru mbuga hiyo. Walimwacha Bahati afurahie mandhari ya huko.

Hatimaye ziara mbugani ilikamilika wakarudi nyumbani. Bahati aliwashukuru sana wazazi wake. Alikuwa amejifunza mengi kuhusu wanyamapori.

9. Kulingana na kifungu, Bahati na wazazi wake walizuru mbuga ipi ya wanyama?

   _____

10. Kifungu kinaonyesha kuwa Bahati ni mwenye maadili kwani

    _____

11. Je, unadhani ni kwa nini mwelekezi alimkataza Bahati kuwapa wanyamapori chakula?

    _____

12. **Hatimaye** ziara ilikamilika mbugani wakarudi nyumbani. Maana ya neno **hatimaye** kulingana na kifungu ni:

    _____

Swali la 13 hadi la 16

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Siku ya Ijumaa asubuhi na mapema, wanafunzi wote wa shule ya Upendo walikusanyika katika gwaride. Walifurahi kukutana na wenzao.

Wanafunzi waliimba wimbo wa Taifa na ule wa Jumuiya ya Afrika mashariki. Baada ya kuimba nyimbo hizo, mwalimu wa zamu alisimama na kuwaamkua, kisha akasema, “Ninachukua fursa hii kuwashukuru nyinyi nyote kwa vile mmedumisha nidhamu wiki hii yote. Ningependa kuwapongeza viranja ambao kila siku husimamia usafi wa madarasa na kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi ametimiza wajibu wake.

Naomba niwashukuru wanafunzi wa Gredi ya Nne kwa kumsaidia mwenzao aliyekuwa ameteguka mguu wakati wa mazoezi ya mchezo wa kandanda. Walionyesha upendo na kuwajali wengine. Wahenga walinena, akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.

Ninamshauri kila mmoja wenu awe mfano mzuri wa kuigwa katika kuwatendea wengine mema. Nawaomba mwendelee kuwaheshimu walimu na wenzenu. Mkifanya hivyo, shule yetu itakuwa mahali penye amani, upendo na ushirikiano.

Nawatakia siku njema!”

13. Kulingana na kifungu, wimbo wa taifa na ule wa Jumuiya ya Afrika Mashariki huimbwa wakati upi?

_____

14. Ni tendo gani katika kifungu linaloonyesha kuwa viranja ni wenye kuwajibika?

_____

15. Unadhani wanafunzi wa Gredi ya Nne walimsaidia vipi mwanafunzi aliyeteguka mguu?

_____

16. Mwalimu aliwaomba wanafunzi waendelee kuwaheshimu walimu na wanafunzi wenzao. Je, angetumia methali gani kupitisha ujumbe huo?

_____

ZOEZI 4

MATUMIZI YA LUGHA

17. Kadi zifuatazo zina meneno mbalimbali. Chagua kadi yenye nomino pekee.

A	B	C
jeshi kitabu	zulia mwerevu	cheza darasa

18. Jaza nafasi kwenye jedwali lifuatalo. Fuata mfano uliopewa.

Kitabu changu kitanifaa.	Vitabu vyetu vitatufaa.
_____	Watoto hawa wanafagia sebuleni.

19. Kamilisha sentensi hii kwa neno linalofaa kutoka kwenye mabano.

Baba amelima shamba.

Shamba _____na baba. (limelima, limelimwa, limelimia)

20. Katika picha hii,

Mbwa amelala _____ mti. (chini ya, ndani ya)

21. Juma amemtembelea shangazi. Kwa hivyo, **yeye** amemtembelea shangazi.

    Maria na Neema wanakula matunda.

    Kwa hivyo, _____wanakula matunda. (nyinyi,wao)

22. Neno, **shule** katika sentensi, **Shule yetu ni safi**, ni nomino. Pigia mstari kielezi katika sentensi ifuatayo:

    Daktari hutibu vizuri.

    _____

23. Urefu ni kwa mlingoti na nyeupe ni kwa _____

24. Neno **mti** liko katika ngeli ya U-I

    Je, neno **jino** liko katika ngeli gani?

    _____

25. Jaza nafasi kwa kuchagua kiambishi sahihi. Fuata mfano.

    Seremala alitengeneza meza juma lililopita.

    Seremala a____tengeneza viti juma lijalo. (me, ta)

26. Unganisha sentensi zifuatazo ziwe sentensi moja. Tumia kiunganishi **na**.

    Juma anacheza mpira. Rono anacheza mpira.

    _____

27. Kanusha sentensi ifuatayo:

    Neema anakariri shairi.

    _____

28. Kuna maneno yanayokaribiana kimatamshi kama vile **fua, vua**. Andika neno linalokaribiana kimatamshi na neno, **baba**.

    _____

29. Umemuaga rafiki yako ukienda kulala.Umemwambia Alamsiki! Je, atatumia neno gani kukujibu?

_____

30. Rafiki yako hatii bidii masomoni. Andika methali ambayo utamwambia ili kumshauri.

ZOEZI 5: KUANDIKA

31. Andika insha kuhusu:

SHULE YANGU

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.